TANGAZO LA SERIKALI NA ..... la tarehe .....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290)

_____

SHERIA NDOGO

_____

Zimetungwa chini ya kifungu 7(1) na 16(1)

_____

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI ZA MWAKA, 2017

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, 2017.

Tarehe ya kuanza kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitaanza kutumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kuanzia tarehe ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi:-

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi au Kaimu wake.

"Afisa Mhidhiniwa" maana yake ni Afisa yoyote aliyeidhinishwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi.

"Ada ya kutua" maana yake ni ada inayolipwa na mtu anayeleta bidhaa au kutoa bidhaa ndani ya eneo la Halmashauri kwa kutumia usafiri wa maji, anga au nchi kavu.

"Mtu" maana yake ni mtu wa kawaida au taasisi au shirika au kampuni na anaweza kuwa mmoja au zaidi.

"Mazao ya majini" inajumuisha samaki, dagaa, magamba ya samaki, na viumbe vyote vyenye asili ya majini.

"Tenga" maana yake ni kifaa chochote ikijumuisha ndoo, debe au kifaa chochote cha kiasili kinachotumika kupima au kubebea samaki au mazao ya majini.

"Vituo vya kutua" maana yake ni maeneo yalioainishwa kuwa ya kutua pembezoni mwa ziwa au ndani ya eneo la Halmashauri na inajumuisha mialo, maduka, masoko, minada, ghala na maeneo mengine ambapo wafanya biashara na wasafirishaji wa bidhaa wanatua kupakua au kupakia, kuuza au kununua bidhaa, mazao ya viwanda, au mazao ya chakula kwa ajili ya shughuli za kibiashara, pia inajumuisha sehemu yoyote yenye kizuizi cha Halmashauri.

"Mnara wa mawasiliano" maana yake ni mnara uliowekwa kwa ajili ya kuwezesha mawasilino ya simu, radio, au televisheni ndani ya eneo la Halmashauri.

"jengo" maana yake ni nyumba iwe imekamilika kujengwa au la; iliyojengwa kwa mawe, matofali mabichi au ya kuchoma, matofali ya sementi au nguzo imara na ambayo imeezekwa kwa bati, vigae au asbestos au makuti kwa majengo ya biashara.

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi toka Halmashauri ya kufanya shughuli yoyote iliyobainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

"maeneo maalumu" inajumuisha maeneo yaliyopimwa kwa mujibu wa sheria au yaliyotengwa kwa ajili ya kufanyia shughuli maalumu chini ya sheria Ndogo hizi.

"utamaduni" maana yake ni shughuli za ngoma za asili, mziki, maigizo, mazingaombwe, sinema na michezo.

"Boti" maana yake ni chombo cha majini kinachoendeshwa kwa kutumia injini iliyopachikwa au kujengewa ndani ya chombo hicho.

"mtumbwi" maana yake ni chombo cha majini kinachoendeshwa kwa kutumia joshi au kasia.

Ada na ushuru wa mazao ya majini, viwanda na kilimo

4. (1) Kutakuwepo na malipo ya ada na ushuru kwa mazao yote ya majini, bidhaa za viwandani na bidhaa za kilimo, kama ilivyobainishwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kila mtu atakaye pakua mizigo au kupakia mizigo kwenye vituo vya kutua ndani ya Halmashauri atatakiwa kulipia ushuru kwa viwango vilivyoainishwa katika **Jedwali la Kwanza 'A'** la Sheria Ndogo hizi.

(3) Itakuwa marufuku kwa mfanyabiashara yoyote kupakia mzigo wenye uzito zaidi ya viwango vilivyobainishwa katika Sheria Ndogo hizi na ikibainika, Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza mhusika faini kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Kibali cha kusafirisha bidhaa

5. (1) Kila mtu atakayesafirisha bidhaa toka Halmashauri kwenda nje ya Halmashauri atapatiwa kibali cha kusafirisha bidhaa, kama kilivyoainishwa katika **Jedwali la Kwanza 'B'** baada ya kulipia ushuru ulioainishwa katika kifungu cha 4(2) cha Sheria Ndogo hizi.

(2)Kila mfanyabiashara wa mazao atawajibika kuwa na kibali halali cha kusafirisha mazao nje ya nchi au ndani ya wilaya, na endapo mazao hayo yatasafirishwa wakati kuna

amri halali ya kutofanya hivyo, mhusika atakuwa ametenda kosa.

(3) Endapo mtu yeyote atakiuka kifungu cha 5(2) cha Sheria Ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na mkurugenzi atakuwa na haki ya kumtoza faini ya papo kwa hapo isiyozidi Tsh.300,000/= kwa kila kosa baada ya mhusika kukiri kutenda kosa hilo kwa maandishi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na mali hiyo itatakiwa kurudishwa mahali ilipotokea.

Vizuizi

6. (1) Halmashauri inaweza kuweka kizuizi katika eneo lolote ndani ya eneo la Halmashauri kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Ada ya maegesho ya magari/ mitumbwi/ boti kwenye vituo vya kutua

7. (1) (i) kutakuwepo na ada ya maegesho ya mitumbwi/boti katika mwalo, kivuko au gati na ada hiyo italipwa kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katiak **Jedwali la Pili 'A'** la Sheria Ndogo hizi.

(ii) mitumbwi au boti zinazofanya kazi ni lazima ziegeshwe katika maeneo maalum yaliyotengwa kwa shughuli hiyo na mitumbwi mibovu au ambayo haifanyi kazi haitaruhusiwa kuegeshwa katika eneo la maegesho lililotengwa.

(2) Kutakuwepo na ada ya maegesho ya magari ya biashara katika maeneo ya magulio, mialo, masoko na minada kwa mujibu wa **Jedwali la Pili 'B'** la Sheria Ndogo hizi.

Ushuru katika magulio,ma soko na mialo

(3) Kutakuwepo na ushuru utakaotozwa katika masoko, magulio na mialo katika eneo la Halmashauri ambao utalipwa kwa mujibu wa **Jedwali la Pili 'C'** la Sheria Ndogo hizi.

Ushuru wa mazao ya misitu

(4) Kutakuwepo na ushuru wa mazao ya misitu ambao utatolewa baada ya kulipia kibali kwa mujibu wa **Jedwali la Pili 'D'** la Sheria Ndogo hizi.

Uchimbaji wa mitaro barabarani

8. (1) Hairuhusiwi mtu yoyote kuchimba barabara au kupitisha mtaro barabarani bila kibali cha Halmashauri ambacho kitatolewa baada ya mhusika kulipia ada kama ilivyoainishwa katika **Jedwali la Tatu** la Sheria Ndogo hizi, na atatakiwa kurejesha barabara kwenye hali yake ya asili kwa viwango vitakavyoafikiwa na Halmashauri.

(2) Mtu yeyote atakayechimba barabara au kuweka tuta

barabarani bila kibali atatakuwa ametenda kosa na Mkurugenzi atakuwa na mamlaka ya kumtoza faini ya Tsh. 200,000/= baada ya kukiri kwa maandishi utendaji wa kosa hilo.

Ada ya upangaji wa nyumba za Halmashauri kwa shughuli za biashara na makazi

9. (1) Vyumba vya biashara katika majengo yanayomilikiwa na Halmashauri vitalipia kodi ya pango ya Tsh. 5,000/= (Elfu Tano) kwa kila eneo moja la mraba ($1M^2$) baada ya wahusika kuingia katika mkataba wa upangaji wa kila mwaka.

(3) Nyumba za makazi za Halmashauri zitatozwa kodi ya pango kwa viwango vitakavyotolewa na Halmashauri na kubainishwa katika mkataba kwa kulingana na thamani ya nyumba na eneo ilipo.

Matangazo ya biashara

10. (1) Kila mfanyabiashara katika eneo la Halmashauri atawajibika kuweka bango la biashara na bango hilo litatakiwa kulipiwa ada ya kila mwaka kwa mujibu wa **Jedwali la Nne 'A'** la Sheria Ndogo hizi.

Ada ya shughuli za utamaduni

(2) Hairuhusiwi kutangaza matangazo yoyote ya biashara ndani ya eneo la Halmashauri isipokuwa kwa kibali maalumu kitakachotolewa baada ya kulipia kiwango kilichoainishwa katika **Jedwali la Nne (B)** la Sheria Ndogo hizi.

11. (1) Hakuna shughuli zozote za kiutamaduni zitakazofanyika au kuendeshwa katika eneo la Halmashauri bila kibali kitakachotolewa na Halmashauri kwa maandishi kikionesha jina la mwombaji, tarehe ya kuanza na kuisha kwa kibali, eneo la kufanyia shughuli za kiutamaduni na ada ya kibali ilyolipiwa.

(2) Halmashauri itatoza ada ya kufanya shughuli za kiutamaduni kwa mujibu wa **Jedwali la tano** la Sheria Ndogo hizi.

(3) Kila mtu atakayepewa kibali cha kuendesha shughuli za utamaduni atahakikisha shughuli zote za sherehe au hafla zinafungwa saa 06:00 usiku.

(4) Mkurugenzi atakuwa na mamlaka ya kumtoza faini isiyozidi Tsh. 300,000/= mtu yeyote atakayekutwa akiendesha shughuli za utamaduni bila kibali au kuzidisha muda wa kufanya sherehe.

Matumizi ya

12. Wanyama wote watatakiwa kuchinjwa kwenye maeneo ya

machinjio/ maeneo maalumu

machinjio au maeneo maalum yatakayoainishwa na Halmashauri.

13. (1) Kila mnyama atakayechinjwa atatozwa ada ya machinjio kwa viwango vilivyoainishwa katika **Jedwali la sita** la Sheria Ndogo hizi.

(2) Wanyama wote watatakiwa kufanyiwa ukaguzi kabla na baada ya kuchinjwa na watalipiwa ada ya ukaguzi kwa mujibu wa jedwali la Sita watakaosafirishwa watalipiwa ada kwa mujibu wa **Jedwali la sita** la Sheria Ndogo hizi.

Tangazo la Serikali Na. 225/2015

(3) Wanyama watakaosafirishwa ndani na nje ya Halmashauri, pamoja na vyakula vya mifugo, watalipiwa ushuru kama ilivyoainishwa katika sheria ya ”the Animal Diseases (Animals and Animal Products Movement Control) Ammendment), 2013”.

Sheria Na. 16/2003 na Sheria Na. No. 17 ya 2003

(4) Kwa yeyote atakayechinja nyama sehemu ambayo hairuhusiwi atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa mujibu wa sheria zinazohusiana na mifugo.

(5) Mifugo yote inayopelekwa machinjioni au kwenye vituo vya kutua au kusafirishwa kwa namna yoyote ile itatakiwa kupitia katika maeneo ya vivuko vilivyowekwa barabarani au kwa kutumia magari, na atakaye kiuka matakwa ya kifungu hiki Mkurugenzi atamtoza faini ya Tsh. 10,000/= kwa kila mfugo utakaokutwa unaswagwa barabarani.

Kibali cha ujenzi na ada ya mnara

14. (1) Kila mtu kabla ya ujenzi wa mnara wa mawasiliano atatakiwa kuomba kibali cha kujenga mnara ndani ya eneo la Halmashauri na kulipia ada ya Tsh. 200,000/= na Mkurugenzi ataingiza mnara huo katika Rejista ya Minara itakayokuwa wazi kwa ukaguzi wakati wowote ule itakapohitajika na mtu au taasisi yoyote.

(2) Mkurugenzi anaweza kuamuru mmiliki wa mnara wa mawasiliano asitishe kutoa huduma hiyo au asimamishe ujenzi wa mnara endapo itabainika kwamba kumekuwepo na ukiukwaji wa masharti yaliyoko ndani ya Sheria Ndogo hizi.

Vibali vya ujenzi wa majengo

15. Majengo yote ndani ya maeneo maalum yaliyotengwa na Halmashauri yatapewa kibali cha ujenzi kabla ya ujenzi wa jengo.

Maombi ya vibali vya ujenzi

16. (1)Vibali vyote vya ujenzi vitaombwa Halmashauri kwa maombi maalumu ambayo yatambatanishwa na ramani ya

jengo lililochorwa na mtaalam wa majengo anayetambuliwa, nakala ya hati ya kiwanja kinachotegemewa kujengwa/uthibitisho wa umiliki wa eneo, ada ya kibali cha ujenzi pamoja na maelekezo mengine yatakayotolewa na Halmashauri.

(2) Vibali vyote vitalipiwa ada kwa kiwango kilichoainishwa kwenye **jedwali la saba** la Sheria Ndogo hizi.

(3) Ujenzi wa jengo la ghorofa katika maeneo yote ya Halmashauri utaombewa kibali cha ujenzi na kusimamiwa na Mkandarasi aliyesajiliwa na Bodi ya Wakandarasi.

(4) Mwombaji atatakiwa kuanza ujenzi katika muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kupewa kibali.

(5) Kibali cha ujenzi kitakachotolewa kitadumu kwa muda wa miaka mitatu na kinaweza kuwa na masharti yafuatayo:

(i) tarehe ya kuanza nakumaliza ujenzi;

(ii) kulipa ada kwa mujibu wa sheria;

(iii) kufuata marekebisho yoyote yatakayobainishwa kwenye michoro na Afisa muidhiniwa;

(iv) kufuata sheria yoyote ya nchi.

Ada ya ukaguzi wa Afya

17. (1) Kutakuwepo na ada ya ukaguzi wa kiafya ambayo itatozwa katika majengo ya biashara mara mbili kwa mwaka kwa mujibu wa Jedwali la Nane la Sheria Ndogo hizi.

(2)Mkurugenzi atakuwa na mamlaka ya kufunga eneo la biashara endapo mmiliki wa biashara husika atashindwa kutekeleza matakwa ya kifungu hiki.

Uwezo wa kukagua

18. (1) Afisa mhidhiniwa au wakala wa Halmashauri aliyeidhinishwa anaweza kuingia wakati wowote ule katika ardhi, jengo, makaazi au chombo cha usafiri ndani ya eneo la Halmashauri na kukagua au kuhoji kitu chochote kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Mkurugenzi anaweza kumtaka wakala au Afisa muidhiniwa kutoa taarifa yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Utambuzi wa vikundi

19. (1) Vikundi vyote vitakavyosajiliwa vitaingizwa katika Rejista ya Halmashauri na kulipia ada ya usajili Tsh. 15,000/= na kuendelea kulipa ada ya Tsh. 10,000/= kwa mwaka.

(2) Kikundi kitakachoshindwa kutimiza masharti ya

kifungu cha 20(1) hapo juu hakitambuliwa na Halmashauri.

Uteuzi wa wakala Sheria Na. 7/2011

20. Halmashauri, kwa njia ya tenda, inaweza kumteua wakala wa kukusanya ada na ushuru uliobainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi, kwa ujumla wake au kwa shughuli mojawapo, kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2011.

Kosa kwa wakala au watoza ushuru

21. 1) Mtu yeyote au aliyechaguliwa wakala au mtoza ushuru wa Halmashauri ambaye bila sababu za msingi :-

(a) Atashindwa kuleta kumbukumbu za biashara au maelezo anayotakiwa kutoa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(b) Atashindwa kuwasilisha ushuru na ada anayodaiwa kuwasilisha baada ya kukusanya;

(c) Atashindwa kuweka kumbukumbu au taarifa zinazohusu ada na ushuru vinavyolipwa na alivyokusanya;

(d) Atashindwa kutoa taarifa yoyote kwa utafiti au makadirio yoyote ya ushuru na ada vinavyotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(e) Atazuia au kujaribu kuzuia Afisa yoyote aliyeidhinishwa au mtoza ushuru wa Halmashauri au wakala kufanya shughuli zake chini ya Sheria Ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na akidhibitishwa kuwa na kosa atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) Bila kuathiri matakwa ya aya ndogo ya (1) ya kifungu hiki, Halmashauri inaweza kurejesha ada na ushuru uliokusanywa kwa njia ya hati ya kosa la jinai au kwa kufungua madai Mahakamani.

(3) Kama mtu yeyote atapokea ilani ya madai yeye binafsi au kama itakuwa imeachwa kwenye eneo lake la kazi na akashindwa kulipa kiasi daiwa kwa Halmashauri, Halmashauri itaomba mahakama yenye mamlaka 'Summary warrant' kwa fomu iliyotolewa kwenye **jedwali la Tisa** la Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kutoa taarifa

22. (1) Mtu yeyote atakayetakiwa kutoa taarifa yoyote, atatakiwa kuitoa kadiri inavyohitajika na Halmashauri kwa nia ya kupata taarifa ya kukadiria na kuweka makisio ya ukusanyaji wa ada na ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(2) Kwa dhumuni la kupata taarifa, chini ya aya (1) ya Sheria Ndogo hizi, Halmashauri inaweza kumtaka mtu yeyote kufika Halmashauri sehemu na muda utakaopangwa.

Makosa na adhabu

23. (1) Mtu yeyote atakayetakiwa kutoa taarifa chini ya Sheria Ndogo hizi na;

(a) Akadharau au kukataa aua kushindwa bila sababu za msingi kutoa taarifa alivyotakiwa;

(b) Kwa makusudi kupotosha au kujaribu kupotosha Halmashauri kwa namna yoyote ile kuhusu ukusanyaji wa ada na ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi; atakuwa ametenda kosa.

(2) Mtu yeyote ambaye kwa njia moja au nyingine anatakiwa kulipa ada na ushuru chini ya sheria ndogo hizi;

(a) Akakataa, kudharau au kushindwa kulipa ada na ushuru au kulipia ada na ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi na kushindwa kudai risiti inayotambuliwa na Halmashauri;

(b) Kuzuia, kushawishi au kusaidia mtu yeyote kutolipa ada ya ushuru;

(c) Kuzuia Afisa mhidhiniwa au wakala kufanya shughuli zake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(d) Kwa namna yoyote ile akivunja mojawapo ya vipengere vya Sheria Ndogo hizi; atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia, isipokuwa pale ambapo adhabu yake imebainishwa katika kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi, atatozwa faini isiyozidi shilingi Laki Tatu (300,000) au kifungo cha miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Mamlaka ya Mkurugenzi kutoza faini‘ Sura. 287 R:E 2002

24. Mtu yeyote akitenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi anaweza kumuamuru mtu huyo, baada ya kukubali kwa maandishi kuwa ametenda kosa hilo, kwa mujibu wa fomu iliyoko katika jedwali la Tisa la Sheria Ndogo hizi, kulipa kiasi kinachodaiwa pamoja na faini ya kukiuka kipengele chochote cha sheria hii kwa kiwango kisichozidi shilingi Laki Tatu.

Sheria Ndogo zilizofutwa GN.No. 272/2011

25. Sheria Ndogo hizi zimefuta sheria Ndogo zifuatazo:-

(i) Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi ‘Ada na Ushuru’ za mwaka 2011 zimefutwa,

GN.No.
276/2011

(ii) Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi (Vibali vya Ujenzi), 2011 zimefutwa,

Isipokuwa, deni lolote ambalo halijalipwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi litadaiwa kama vile Sheria Ndogo hizi hazijawai kufutwa.

JEDWALI LA KWANZA

(chini ya kifungu cha 4 & 5)

A: USHURU WA KUPAKIA NA KUPAKUA BIDHAA

SEHEMU 'I' Bidhaa za Majini

1.	Kilo moja ya samaki wabichi……	5 %ya bei ya manunuzi
2.	Samaki wakavu:	
	(ii) tenga la saizi ya kati la samaki wakavu kg 21-50 ……..	2,000/=
	(iii) tenga kubwa la samaki wakavu kg 51-100…….	5,000/=
3.	Dagaa	
	gunia la dagaa lenye kg 20-50……..	1,000/=
	gunia la dagaa lenye kg 51-100…… …….	1,500/=
4.	gunia la magamba ya konokono:	
	kg 1-20 …….. ……	500/=
	kg 21-50……..	1,000/= /=
5.	(i) gunia la mabondo kg 1-20……	10,000 /=
	(ii) gunia la mabondo kg 21-50 ……	25,000 /=
	(iii) gunia la mabondo kg 51-100……..	40,000 /=
6.	chakula cha mifugo:	
	(i) gunia lenye kg 1-20……..……..	500/=
	(ii) gunia lenye kg 20-50……	800 /=
	(iii) gunia lenye kg 51-100…….…….	1,000/=

7. Mabini ya samaki ……. 1,000/= kila tani kwa safari

SEHEMU 'II' : Bidhaa za Kilimo

1. Mazoa yote ya biashara ndani ya Halmashauri (isipokuwa ndizi) yatalipiwa ushuru wa asilimia zizizopungua asilimia mbili (2%) na zisizozidi asilimia tano (5%) ya bei ya manunuzi baada ya Azimio la kiwango husika kutolewa na Halmashauri kwa kila mwaka wa fedha kulingana na upatikanaji wa zao husika na kwa kuzingatia sheria nyingine elekezi za bei ya mazao.
2. Upakiaji wa magunia ya mazao hautatakiwa kuzidi kg 100

Sehemu 'III' : Bidhaa za ndizi:

		ushuru kwa kila mkungu
1.	Aanayesafirisha kwenda nje ya wilaya ……	500/=
2.	Anayeuza ndani ya wilaya…….	300/=
3.	Mshare (Njoge) anayesafirisha nje ya wilaya...…….	500/=
4.	Mshare (Njoge) anayeuza ndani ya wilaya……	300/=
5.	Ndizi aina ya Gonja……..	500/=.
6.	Ndizi sukari (akanana)……..	200/=

SEHEMU 'III' Kupakia na Kupakua Bidhaa za viwandani ndani ya eneo la Halmashauri

1. Gari la bidhaa za viwanda litalipia Tsh..... 1,000/= kwa kila tani kwa kila bidhaa

2. Gari la mafuta ya taa, au diesel, au petrol, au gesi au bidhaa nyingine za mlipuko .....Tsh.1,500/= kwa kila tani

B: Kibali cha kusafirisha bidhaa kutoka katika halmashauri ya wilaya ya Missenyi

Kibali kinatolewa kwa Ndugu…….
Mmiliki wa Leseni yenye Na…….. toka …….
Kwa ajili ya kusafirisha bidhaa toka Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kwenda ……
kwa bidhaa yenye maelezo yafuatayo:

Aina ya bidhaa inayosafirishwa	Idadi/Ujazo wa mzigo	Ada na Ushuru uliolipwa Halmashauri	Na. ya risiti	Mahali bidhaa inapopelekwa	Tarehe ya kusafirisha bidhaa

Kibali cha kusafirisha bidhaa hizi kimetolewa leo hii tarehe……..mwezi…….mwaka……...
Jina la Afisa mhidhiniwa……
Sahihi…….
Cheo……

Jina la mwombaji wa kibali……
Sahihi……..
Tarehe…….

JEDWALI LA PILI

(chini ya kifungu cha 7)

Sehemu 'A': Ada ya Maegesho ya Mitumbwi na Boti

1.Mitumbwi……. 200 /= kila unapoegeshwa kwa siku
2. Kalua/Ngama….. 500 /= kila inapoegeshwa kwa siku
3. Kivuko 'Ferry'…. 500/= kila inapoegeshwa kwa siku
4. Meli Ndogo……. 2,000/= kila inapoegeshwa kwa siku
5. Boti iliyobeba sanduku za kubeba samaki……. 1,500/= kila inapoegeshwa kwa siku
6. Makontena…… 5,000/= kila inapoegeshwa kwa siku
7. Mitumbwi ya kusafirisha abiria…… 500 /= kila safari

Sehemu B: Ushuru wa maegesho ya magari ya biashara kwenye magulio, mialo, masoko

1.Gari lenye tani 1-7…… 2,000/= kwa siku
2. Gari lenye tani 7-10…… 5,000/= kwa siku
3. Gari la zaidi ya tani 10… 10,000/= kwa siku
4. Pikipiki…… 500/= kwa siku
5. Magari binafsi yasiyo ya biashara… 500/= kwa siku

Sehemu C: Ushuru katika Masoko, Magulio na Mialo kwa siku

1. Biashara ya nguo za mitumba……. 1,000/=
2. Biashara ya nguo za maduka…… 1,000/=
3. Biashara ya viatu vya mitumba…… 1,000/=
4. Biashara ya mamalishe…… 1,000/=
5. Biashara ya vileo……. 2,000/=
6. Biashara ya kuuza nyama…… 5,000/=
7. Michezo mbalimbali……. 2,500/=
8. Biashara za bidhaa za urembo……1,000/=
9. Biashara ya vyombo vya ndani……. 1,000/=
10. Biashara ya samani mbalimbali…… 1,000/=
11. Biashara ambazo hazijatajwa…….. 2,000/=

Sehemu 'D':

1. Mkaa ……. 1,000/=
2. Mbao…- 500/=kila ubao uziozidi futi 12 za 1x8, 1x10, 2x3, 2x6
   - 300/= kila ubao wenye vipimo vya 2x2,1x4 kwa urefu usiozidi futi 12……..300/=
   - kila futi itakayoongezeka Tsh.50/=
3. Kuni… - Tani 1-5 Tsh. 30,000/= ;
   - Tani 5-10 Tsh.50,000/=;
   - zaidi ya Tani 10 Tsh. …...1,000/= kwa kila tani itakayoongezeka.
4. Nguzo…….. 300/=kila moja
5. Gogo……. 3,000/= Kila mita za ujazo
6. Fito… - Tani 0-5 ……. 20,000/=
   - Tani 6-10…… 30,000/= na Tsh.500/= kwa kila Tani itakayoongezeka
7. Asali…….. …… 500/= kila lita tano za ujazo
8. Nta…… 500/=kwa kila kilo
9. Kibali cha kukata mti au kuvuna mti……. ….. 1,000/=Kila mti
10. Mabanzi…… 200/= kila moja

JEDWALI LA TATU

(chini ya kifungu cha 8(1))

MAOMBI YA KUCHIMBA/KUPITISHA MTARO KWENYE ENEO LA BARABARA

1. Barabara za lami…….. 100,000/=
2. Barabara za kawaida…… 50,000/=

JEDWALI LA NNE

(Zimetengenezwa Chini ya Kifungu cha 10)

SEHEMU A:

(a) Ada ya Mabango kwa mwaka

(i) Kila bango linalotoa mwanga litalipia 6/=kwa kila M^2 1 kwa mwaka

(ii) Kila bango ambalo halitoi mwanga litalipia 5/= kwa kila M^2 1 kwa mwaka

(b) Matangazo yaliyobandikwa kwenye ukuta/kuchorwa kwenye ukuta yatalipia 5/=kwa kila M^2 1 kwa mwaka

JEDWALI LA TANO

(Zimetengenezwa Chini ya Kifungu cha 11(2))

Ada ya sughuli za utamaduni

1. Disco siku za sikukuu na mwisho wa juma 20,000/= kwa siku
2. Tiba za jadi 30,000/= kwa mwaka
3. Michezo ya sanaa za maonyesho ngoma, maigizo,sarakasi, michezo ya nguvu, nyimbo 5,000./= kwa siku katika taasisi na Tsh.10,000/= kwa siku katika kumbi
4. Shughuli za sanaa za ufundi (uchoraji) picha, upakaji rangi, vinyago10,000/= kwa onyesho
5. Kunasa kanda za sauti kwa vikundi wakati wa mashindano ama shughuli iliyoandaliwa na Halmashauri 10,000./= kwa siku
6. Vikundi vya sanaa za ufundi 10,000/= kwa mwaka.
7. kuendesha promotion katika bar/hotel 20,000/= kwa siku
8. wasambazaji wa cable za runinga (TV) 30,000./= kwa mwezi
9. Kucheza meza za poll10,000/= kwa mwezi
10. Sehemu za makumbusho au za kihistoria kwa mtu mmoja:
    i. Mtu mzima raia ……1,000 /=
    ii. Mtu mzima asiye raia ……Us $ 10
    iii. Mwanafunzi wan je ya nchi …….Us $ 5
    iv. Mwanafunzi wa ndani ya nchi…Bure

11. Kuendesha utafiti wa mambo ya kale na tafiti nyingine zinazofanana na hizo kwa miezi mitatu:
    i. Raia 50,000/=
    ii. Asiye raia Us $ 70

Ushuru mwingine:

i.	Molasses……..	200/= kwa kila lita
ii.	Ushuru wa mnada wa jumla wa kitu kinachonadiwa…	5% ya bei yam nada
iii.	Choo cha umma……	300/= kwa siku
iv.	Kibali cha kufyatua matofali ……..	20,000/= kwa miezi sita

JEDWALI LA SITA

(Zimetengenezwa Chini ya Kifungu cha 13)

1. Ushuru wa kuchinja mifugo

Mifugo	**Machinjioni**	**Maeneo maalum (slaughter slub) kwa kila mfugo**
Ng'ombe	3,500/=	2,000/=
Nguruwe	1,500/=	1,000/=
Mbuzi	1,500/=	1,000/=
Kondoo	1,500/=	2,000/=

2. Ada ya ukaguzi wa wanyama (ukaguzi wa awali masaa 12 kabla ya kuchinja):-
   (1) Ng'ombe ……..…..… 500/=
   (2) Mbuzi/ Kondoo……..……..… 300/=
   (3) Nguruwe……..…… 300/=

3.kodi ya jengo la kutunza ngozi kwa mwezi……. 30,000/=

4. Ada ya ukaguzi wa nyama baada ya kuchinja:-.
   (1) Ng'ombe ……..……. 1,000/=
   (2)Mbuzi/ Kondoo……..…….. 300/=
   (3)Nguruwe……..……. 300/=

5. Ushuru wa Mifugo (mnadani)

Aina ya mifugo

(1) Ngombe…… . 5,000/= kila mmoja
(2) Mbuzi/kondoo…… 2,000/=kila mmoja
(3) Nguruwe ……. 2,000/=kila mmoja

JEDWALI LA SABA

(Zimetengenezwa Chini ya Kifungu cha 17(2))

ADA YA VIBALI VYA UJENZI

ENEO LA SAKAFU LINALOZIDI META ZA ENEO (M^2)	**ENEO LA SAKAFU LISILOZIDI META ZA ENEO (M^2)**	**VIWANGO VYA ADA**
	45.45	15,000/=
45.45	92.01	20,000/=
92.01	139.35	30,000/=
139.35	185.81	45,000/=
185.81	231.274	50,000/=
231.274	278.71	70,000/=

1.Ongezeko la ada kwa kila meta moja ya mraba zaidi ya meta za mraba 278.71 ni shilingi 150/=
2. Upanuzi wa majengo pia utafuata kiwango hiki
3. Mabadiliko ya kuta za nje za jengo kwa upanuzi wowote
Utatozwa shilingi 40,000/= kima cha chini.

JEDWALI LA NANE

Limetengenezwa chini ya kifungu cha 18

Ada ya ukaguzi wa afya

1. Nyumba za starehe (baa, vilabu vya pome za kienyeji na nyumba za kulala wageni) …..5,000/= kila baada ya miezi sita
2. Maduka ya bidhaa…… 2,000/= kila baada ya miezi sita
3. Nyumba za kutengeneza na kuuzia vyakula na nyama choma… 3,000/=kila baada ya miezi sita
4. Ukaguzi wa maombi ya kufungua biashara……. 10,000/= kila ombi
5. Ukaguzi wa maombi ya kufungwa biashara baada ya ukaguzi ili kufunguliwa upya 10,000/=.kila ombi
6. Ukaguzi wa viwanda vikubwa…… 100,000/=
7. Ukaguzi wa viwanda vya kati……. 50,000/=
8. Ukaguzi wa viwanda vidogo…….. 10,000/=
9. Bucha ……. 3,000/=
10. Machinjio…… 3,000/=
11. Saluni……. 2,000/=

JEDWALI LA TISA

Limetengenezwa chini ya kifungu cha 25

Mimi……Nakiri mbele ya ……Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kwamba mnamo tarehe ……..ya mwezi……..mwaka……..Niltenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu …….cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi za mwaka 2017. Nipo tayari kulipa kiasi cha ada/ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi atatekeleza mamlaka yake aliyopewa chini ya Sheria Ndogo tajwa. Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe……. Sahii……..

JEDWALI LA KUMI

(Zimetengenezwa Chini ya Kifungu cha 21(3))

FORM OF SUMMARY WARRANT OF ATTACHMENT AND SALE

To the Court Broker,

……

…….

This is to command you to attach and hold the movable / immovable property of

……

……. who shall pay you the sum of Tshs……. Being the rate due and owing by the said …… together with interest at the date ……and the cost of this attachment and after giving fourteen days notice by affixing the same to this court house and making due proclamation to sell auction aforesaid. You are further commanded to return this warrant on or before the ……. Day of ……with an endorsement certifying the manner in which it has been executed or reasons why it has not been executed.

Given under my hand and the seal of this Court this …….day of ……..20……

…….

Resident Magistrate

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kilichofanyika tarehe ……. na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya-

……..
PROJESTUS K. TEGAMAISHO
MWENYEKITI
HALMASHAURI YA WILAYA
YA MISENYI

……
LIMBE B. MAURICE
MKURUGENZI WA
HALMASHAURI YA WILAYA
YA MISSENYI

NAKUBALI,

……
GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
WN OR - TAMISEMI

DODOMA
Tarehe ……..